**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Arusha.*
*07 Machi, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## RAIS SAMIA ASHIRIKI MKUTANO WA 25 WA WAKUU WA NCHI WANACHAMA WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo ameshiriki katika Mkutano wa 25 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) uliofanyika jijini Arusha.

Mkutano huo uliwakutanisha Marais Mhe. William Samoei Ruto wa Jamhuri ya Kenya; Mhe. Évariste Ndayishimiye wa Jamhuri ya Burundi; Mhe. Yoweri Kaguta Museveni wa Jamhuri ya Uganda; na Mhe. Hassan Sheikh Mohamud wa Jamhuri ya Shirikisho la Somalia; huku Jamhuri ya Rwanda ikiwakilishwa na Waziri Mkuu, Mhe. Justin Nsengiyumva kwa niaba ya Rais Paul Kagame; Jamhuri ya Sudan Kusini ikiwakilishwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mhe. Balozi Monday Semaya Kumba kwa niaba ya Rais Salva Kiir Mayardit; na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ikiwakilishwa na Waziri wa Ushirikiano wa Kikanda, Mhe. Didier Mazenga Mukanzu kwa niaba ya Rais Félix Antoine Tshisekedi Tshilombo, kwa lengo la kujadili maendeleo ya ushirikiano wa kikanda, biashara na ustawi wa wananchi wa Afrika Mashariki.

Katika mkutano huo, Wakuu wa Nchi Wanachama wamemteua Balozi Steven Patrick Mbundi wa Tanzania kuwa Katibu Mkuu mpya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa kipindi cha miaka mitano kisichoweza kuongezwa.

Balozi Mbundi, ambaye hadi wakati wa uteuzi wake alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ameapishwa rasmi wakati wa mkutano huo na anatarajiwa kuanza majukumu yake kuanzia mwezi Aprili, 2026.

Katika hatua nyingine, Wakuu wa Nchi Wanachama wa EAC wamezindua rasmi Mkakati wa Saba wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (2026/27 – 2030/31) unaolenga

kuimarisha ujumuishaji wa kikanda na kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Viongozi hao pia wamezindua mfumo wa dhamana ya forodha wa kikanda *(East African Community Customs Bond)* unaotarajiwa kurahisisha usafirishaji wa bidhaa mipakani na kupunguza gharama za shughuli za kibiashara kwa nchi wanachama.

Aidha, mkutano huo umepokea na kujadili taarifa ya Baraza la Mawaziri la EAC kuhusu utekelezaji wa programu na miradi ya Jumuiya kwa kipindi cha kuanzia tarehe 30 Novemba, 2024 hadi 31 Desemba, 2025, iliyoonesha ongezeko la biashara ndani ya jumuiya pamoja na hatua mbalimbali zinazochukuliwa ili kuondoa vikwazo vya biashara baina ya nchi wanachama na kuimarisha miundombinu ya kikanda.

Wakuu wa Nchi Wanachama pia wamefikia maamuzi mbalimbali ya kuimarisha uendeshaji wa Jumuiya hiyo ikiwemo kupitisha mfumo mpya wa michango ya nchi wanachama wa EAC kuanzia tarehe 01 Julai, 2026, ambapo nchi wanachama zitachangia asilimia 50 kwa usawa na asilimia 50 kulingana na uwezo wa uchumi wa kila nchi.

Halikadhalika, wameipongeza Tanzania kwa maandalizi ya mkutano huo na kwa mapokezi mazuri yaliyotolewa kwa viongozi na ujumbe wao wakati wote wa mkutano huo.

Mkutano umehitimisha kwa makabidhiano ya uenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Jamhuri ya Uganda imechukua nafasi ya Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, huku Jamhuri ya Rwanda ikichukua nafasi ya *rapporteur*.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu